**Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room**

**Episode 02 – "Corruption Needs a Scapegoat"**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller**

**Proofreading: Charlotte Collins**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

Intro & Outro:

- NARRATOR

Scene 1:

- Jeffrey (MALE, 58)
- Mrs Mbata (FEMALE 55)
- Chairman (MALE, 65)
- NARRATOR

Scene 2:

- Isaac (MALE, 22)
- Policeman (MALE, 25)

Scene 3:

- Jennifer (FEMALE, 55)
- Isaac (MALE, 22)

- Sylvia (FEMALE, 19)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Alfayo (MALE, 58)

**Intro:**

**0. Narrator:**

Karibu kwenye makala nyingine ya **Noa Bongo Jenga Maisha yako**. Hii ni sehemu ya pili kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Ufisadi kwa jina “**Tembo Chumbani**”. Katika kipindi hiki tunafuatilia maisha ya familia ya Odhiambo, na jinsi ufisadi ulivyojikita mizizi na kuathiri maisha ya watu miongoni mwa mataifa mengi barani Afrika. Ni vipi mtu anaweza kuishi maisha ya kawaida bila ya kujihusisha na ufisadi?

Katika kipindi kilichotangulia, Lydia anashangaa baada ya kufahamu kwamba wazazi wa rafiki yake wa karibu, wamekuwa wakitoa hongo kwa walimu ili mtoto wao aweze kupata matokeo bora shuleni. Kwa upande mwengine, babake Lydia, Alfayo Odhiambo, anapata habari kwamba kampuni yake imekuwa ikiuza mita za umeme kwa kampuni bandia. Hatimaye kampuni yake hiyo, inahusishwa moja kwa moja na genge la watu walaghai wenye uwezo wa kifedha ambao wanahusishwa na maovu hayo. Jambo hili linamkasirisha sana Alfayo.

Lakini anatumai rafiki yake Jeffrey anayefanya kazi katika halmashauri ya kupambana na ufisadi ataweza kumsadia kujitoa katika kashfa hii. Lakini kama tutakavyosikia katika kipindi hiki, ufisadi hunawiri na kukita mizizi zaidi kwa kutumia visingizio. Kwa upande wake, Jeffrey naye anakabiliwa na matatizo ya kibinafsi kazini mwake.

## Scene One:

***KW begins***

**1. Atmo:** **Office background noises: typing, telephones ringing**

**2. Jeffrey:** Habari ya asubuhi Bi. Mbata?

**3. Mrs Mbata:** Nzuri. Mwenyekiti wa halmashauri yetu anataka kukuona ofisini mwake. Anakusubiri saa hivi.

**4. Jeffrey:** Sawa ..! Unafununu yoyote kuhusu sababu za yeye kutaka kuniona?

**5. Mrs Mbata:** Hata sina habari. Ila amesema tu ni dharura.

**6. Jeffrey:** Sawa, nitaenda kumuona sasa hivi. Na asante sana Bi. Mbata!

***KW ends***

**7. SFX:** **Door opening and closing**

**8. Chairman:** Habri ya asubuhi Bw Jeffrey. Pita ndani na uketi.

**9. Jeffrey:** Asante sana... **(moves chair to sit down)** Naambiwa unataka kuniona kwa dharura?

**10. Chairman:** Bila shaka. Ni kuhusu suala ambalo linahitaji kujadiliwa kwa makini sana. Mimi mwenyewe naona vigumu, sijui nitaanzia wapi! Nafahamu umekuwa mwanachama mwaminifu katika halmashauri hii tangu tuanze kufanya kazi na wewe. Na ndio sababu naona ugumu sana kulizungumzia suala hili.

**11. Jeffrey:** Ugumu gani?

**12. Chairman:** Sawa Jeffrey, moja kwa moja nitakueleza nilichokuitia hapa. Nimepokea malalamiko kwamba kazi yako hairidhishi hata kidogo. Na mimi nakabiliwa na shinikizo la kukuachisha kazi.

**13. Jeffrey:** Nini? Unataka kunifuta kazi?

**14. Chairman:** Sipendi kulitumia neno hilo! Lakini kama unavyosema hivyo ndivyo nilivyomaanisha, kwamba Jeffrey, tunakufuta kazi.

**15. Jeffrey:** Kwa misingi gani hasa? Navyofahamu mimi nafanya kazi kwa bidii zaidi kuliko wafanyakazi wengine mbali na wewe. Nimeweza kuwasilisha kesi nyingi zaidi za ufisadi katika ofisi hii kuliko ofisa yoyote yule. Na kwanini unataka kunifuta kazi? Na ni nani huyo amekuja kukulalamikia utendaji kazi wangu?

***KW begins***

**16. Chairman:** Ni kweli wewe unajua kwamba unafanya kazi kwa bidii sana Jeffrey, lakini bidii zako hizo bado haziridhishi wengine na ndio sababu ya kuwepo kwa malalamiko haya.

**17. Jeffrey:** Unanishangaza sana! Mimi huwa mtu wa kwanza kufika ofisini, na kuondoka usiku sana. Pengine jambo ambalo

naweza kulaumiwa nalo, ni kesi ambazo uchunguzi wake haujakamilika na hakuna hata mmoja ambaye ameshtakiwa. Lakini hilo si kosa langu!

***KW end***

**18. Chairman:** Samahani lakini halmashauri imekubaliana kwa kauli moja kwamba utendaji kazi wako hauridhishi, hivyo hakuna sababu ya wewe kuendelea kufanya kazi hapa!

**19. Jeffrey:** **(deciding to take the bull by the horns:)** Nadhani haya yote yanatokana na ile kashfa kuhusu sekta ya nishati, ambayo nimeiwasilisha kwa uchunguzi, sivyo? Kwa hivyo, mnashirikiana kujaribu kuficha kashfa hii, sivyo?

**20. Chairman:** Jeffrey Thiongo, unathubutu kuzungumza na mimi hivo! Hata hivyo kashfa inayotajwa hapa ni mambo ya kutunga tu! Haina ukweli wowote! Tulimkabidhi ofisa mwengine wa ngazi za chini kuendelea na uchunguzi wa kesi hiyo na kulingana na uchunguzi wake, hakuna ushahidi wa kutosha mbali na kumshtaki mtu.

**21. Jeffrey:** Imenichukua muda wa miezi sita kuchunguza kesi hiyo! Na nafahamu kila kitu kuhusu kesi hii, na mimi najua kwa hakika kuna ushahidi wa kutosha. Ila kilicho bayana, hakuna mtu mwenye nia ya kufuatilia kesi hii, kwasababu wewe mwenyewe unahofia kupoteza kazi yako.

**22. Chairman:** Samahani, unasema nini?

**23. Jeffrey:** Wewe ni mhusika katika sakata hili, sivyo? Wewe ni mshirika? Najua kuna watu wanaokushinikiza kutupilia mbali kesi hii, lakini nakuhakikishia kwamba lazima kesi hii haitakomea hapa! Unaweza kunifuta kazi ukipenda, lakini ni lazima sakata hili lijulikane!

**24. Chairman:** **(laughs)** Jeffrey, Jeffrey! Wacha mzaha..! Nani atakuamini wewe? Rais labda? Unadhani atanisikiliza mimi au wewe? Sasa una muda wa saa moja kufunga virago, na kuondoka baada ya kukabidhi kitambulisho cha kazini. Na kisha nakutahadharisha. Kuna watu wenye uwezo mkubwa ambao hawataridhika endapo ukiendelea na vitisho vya kufichua

sakata hili Jeffrey Thiongo. Nakushauri uachane na na mambo haya!

**25. Jeffrey:** **(scraping back his chair)** Oh, sidhani itakuwa rahisi kama unavyofikiria. Mimi ni mtu tofauti kabisa. Hii kashfa lazima ifichuke na ole wako usije ukaangamia na kundi zima hilo Bw. mwenyekiti. Lazima nitamuonyesha!

**26. SFX:** **Opens and slams the door**

**27. Narrator:** Mara nyingi suala la ufisadi linapojitokeza, watu waaminifu huwa ndio wanaotumiwa kama chambo! Unapofanya kazi kwa bidii na kujitolea katika kupambana na ufisadi, unaweza kuwa unahatarisha maisha na hata kazi yako, huku ukibaki kujiuliza maswali yasiyoweza kupata ufumbuzi, kama ilivyotokea kwa Jeffrey Thiongo. Tunaona kwamba ufisadi si jambo linaloweza kukabiliwa kwa urahisi. Mara nyingi, kashfa za aina hii huwa zinahusisha watu wa ngazi zote, kuanzia wanasiasa, wafanyabiashara mashuhuri hadi kwa mtu wa chini kabisa. Jeffrey anasisitiza lazima afichue kashfa hiyo. Lakini kumbuka wale wanaojitokeza kufichua kashfa za ufisadi huwa wanahatarisha maisha yao pamoja na familia zao. Je! Jeffrey atakuwa mjasiri wa kudumisha msimamo wake katika kupambana na ufisadi? Hayo ni

baadaye... lakini kwanza tugeukie familia ya Odhiambo. Mtoto wa Alfayo, Isaac, anaelekea nyumbani baada ya kazi....

**Scene Two:**

**28. SFX:** **car driving, radio on**

**29. Isaac:** **(speaking on the phone as he drives)** Ndiyo, ndiyo! Ni sawa Sam, tufanye wikendi. Naweza kuja nyumbani kwako au wewe uje kunitembelea nyumbani kwangu….Ndiyo, hasa.….! Ooooh sikiliza,.....! Samahani tuzungumze baadaye, nadhani maofisa wa usalama wameniona nikiongea na simu. Ahhh Mungu wangu! Wamenisimamisha .. ! Tutaongea baadaye. **(hits steering wheel)** Balaa hili!

**31. SFX/Atmo:** **Opens car window: outside busy traffic on road**

**32. POLICE:** Stakabadhi zako tafadhali!

**33. ISAAC:** Hizi hapa. Bwana Ofisa!

**34. POLICE:** Unaendesha gari huku ukiongea na simu? Hilo ni kosa kubwa! Nataka tuandamane hadi kituoni na tutakushtaki kwa kosa hilo.

**35. ISAAC:** Oh samahani sana Bwana Ofisa, ilikuwa simu ya dharura ndio maana ikanilazimu niipokee!

**36. POLICE:** Kama nilivyotangulia kusema, ni hatia. Utaandamana nami hadi kituo cha polisi.

**37. ISAAC:** Sasa hivi? Lakini huu ni wakati wa msongamano wa magari. Tutakwama barabarani kwa saa nyingi sana.

**38. POLICE:** Hiyo si shida yangu. Umevunja sheria. Hebu nifungulie mlango wa gari na tuandamane hadi kituoni.

**39. ISAAC:** Sawa ...sawa ..pengine tunaweza kuzungumza tukiwa njiani....?

**40. SFX:** **opens car door and closes**

**41. SFX:** **starts the car, drives off**

**42. ISAAC:** Nisikilize...nitaendesha gari kuelekea upande huu wa chini wa barabarani kisha nitapinda .. si unaweza kuchukua .. hizi! Kisha nitakurudisha mahali nilipokuchukua kwenye barabara kuu?

**43. SFX:** **Rustling a banknote**

**44. POLICE:** Samahani lakini "hiki kitu kidogo" hakitanishawishi nisikupeleke kituoni.

**45. SFX:** **Rustling another banknote**

**46. ISAAC:** Sawa, sawa, chukua hata hizi pia..! Tafadhali niachilie..!

**47. POLICE:** Sasa unazungumza! Lakini kumbuka usijaribu tena kuongea na simu wakati unapoendesha gari. Pesa ulizonipa ni kama faini tu.

**48. SFX:** **car stops, car door opens and closes**

## Scene Three:

**49: Narrator:** Isaac anapofika nyumbani, wazazi na dada zake wawili , Lydia na Sylvia wako mezani kwa chakula cha jioni .

**50. SFX:** **Family eating supper. Cutlery clinking, conversation**

**51. SFX:** **Door opens and slams**

**52. ISAAC:** Ahhh, amini usiamini, leo nimepatikana na mafia wa usalama kwa kosa la kuongea na simu huku nikiendesha gari!

**53. JENNIFER:** Ni kosa kubwa kuongea na simu wakati unapoendesha gari! Unajua ni ajali ngapi husababishwa na tabia hiyo, Isaac?

**54. ISAAC:** Mama!

**55. LYDIA:** Kwa hivyo, ukapelekwa hadi kituoni?

**56. ISAAC:** Mimi, Lydia? Nipelelekwe kituoni? Siwezi! Nimewahonga mara moja!

**57. SYLVIA:** Umefanya nini Isaac? Umewahonga! Huo ni ufisadi!

**58. LYDIA:** Sylvia anasema kweli. Huo ni ufisadi. Isaac! Umeniaibisha sana! Wewe ni mwanafunzi wa masuala ya sheria na hivi karibuni utakuwa mwanasheria na huku tayari umeanza kutoa hongo. Hili ndilo tatizo kubwa – Watu wanaopaswa kuwa mstari wa mbele kusimamia sheria, ndio kwanza wanaongoza kwa ufisadi!

**59. ALFAYO:** Ni kweli, Isaac, nakubaliana na Lydia. Wewe ni mwana sheria. Je! Itakuwaje ukianza kufanya kazi, kama saa hii umeanza kutoa hongo...! Ni vipi utaweza kuamua kesi za ufisadi wakati ukianza kufanya kazi ikiwa mwenyewe ni fisadi?

**60. ISAAC:** Ooh hapana! Sasa mnavuka mpaka.

***KW begins*** Hii ni sawa na kulipa faini tu!

**61. SYLVIA:** Sawa hata kama ni faini lakini lazima ulipe mahakamani au katika kituo cha polisi ili pesa hizo ziweze kuingia katika hazina inayostahili. Na wala sio kwa mifuko ya watu binafsi.

**62. ISAAC:** Una uhakika pesa zinazolipwa baada ya mtu kutozwa faini zinafika barazani? Wewe unaota Sylvia!

**63. SYLVIA:** Sawa lakini huwezi kulinganisha ufisadi huo na rushwa ya hadharani. Mtu anapolipa faini mahakamani hawezi kuhusishwa moja kwa moja na kitendo cha ufisadi.

***KW ends***

**64. ALFAYO:** Isaac. Iwapo kweli unataka kuwa mwanasheria, basi una safari ndefu sana, na unapaswa kuanza kutafakari athari za uovu huu. Dada zako wanasema ukweli. Vita dhidi ya ufisadi humu nchini vitategemea juhudi za watu kama wewe. Lazima uwe mfano bora wa kuigwa.

**End of scene**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**65. NARRATOR :** Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya leo kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Ufisadi kwa jina "**Tembo chumbani**". Familia ya Odhiambo haiwezi kupuuza jinamizi hili nyumbani mwao, licha ya ukweli kwamba unaathiri pakubwa maisha yao. Katika kipindi kitakachofuata, mama watoto pia anakabiliwa na vishawishi vya kula rushwa ili kuwasaidia baadhi ya wanafunzi kupata matokeo bora. Je ni vipi alikabiliana na vishawishi hivi?

Ungana nasi tena kwa kipindi kinachofuata ufahamu yatakayojiri kwenye mfululizo wa mchezo huu kuhusu ufisadi. Na ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki unaweza kufanya hivyo kupitia mtandao wetu wa dw.de/lbe. Pia ukiwa na maoni unaweza kuyatuma kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!